TANGAZO LA SERIKALI Na. 27 la Tarehe 17/02/2017

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 153

# SHERIA NDOGO ZA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE ZA MWAKA 2017

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1.Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Mlele 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2.Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.

Tafsiri

3.Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-
“Ada ya Mtumiaji” maana yake ni ada inayotozwa na Hospitali, kituo cha afya au zahanati, kwa ajili ya huduma ya afya inayotolewa kwa mtumiaji;
“Asasi” maana yake ni pamoja na shule, vyuo, vikundi mbalimbali vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria au asasi yoyote itakayokuwa imekubaliwa na kuidhinishwa na Bodi;

Sura ya 287

“Bodi’’ maana yake ni Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mlele;

“Huduma za afya” maana yake ni huduma zote za afya zinazotolewa na hospitali za Serikali na watu binafsi, na zinajumuisha huduma nyingine za afya zilizoanzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za afya ikiwa ni pamoja na vituo vya

afya na Zahanati;

“Kadi” maana yake ni kadi itakayotolewa na Bodi kwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

“Kaya” maana yake ni :

(a) mama, baba, watoto wenye umri chini ya miaka kumi na nane;
(b) mwanachama yeyote aliyefikisha umri wa miaka kumi na nane au zaidi na awe na mtoto au bila mtoto mwenye umri wa miaka kumi na nane;
(c) Taasisi au asasi yoyote.

“Kituo cha huduma kilichoteuliwa” maana yake ni kituo kinachotoa huduma za afya na ni pamoja na kituo chochote kilichoanzishwa au kinachoendeshwa kwa malengo ya kutoa huduma za afya kiwe kinamilikiwa na Halmashauri, Serikali, asasi ya kidini, mtu au watu binafsi ambacho kinahusika na mfuko wa Afya ya Jamii.

“Malipo ya huduma” maana yake ni malipo yanayotozwa na kituo cha tiba, kilichoteuliwa kwa watu ambao sio wanachama, wanapopatiwa huduma za afya katika kituo hicho;

“Mchango au ada ya mwanachama” maana yake ni mchango wa hiari utakaotolewa na wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

“Mfuko au Mfuko wa Afya ya Jamii” (CHF) maana yake ni mfuko wa afya ya jamii ulioanzishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

“Mganga Mkuu wa Wilaya” maana yake ni daktari ambaye ni msimamizi mkuu wa shughuli za huduma za afya katika Halmashauri.

“Mwanachama” maana yake ni kaya inayochangia kwenye Mfuko wa Afya ya Jamii;

“Tele kwa Tele” maana yake ni mkataba unaoeleza wajibu wa Halmashauri wajibu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika

*Tangazo la Serikali Na.27 (linaendelea)*

utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

Mfuko wa Afya ya Jamii

4. (1) Kutakuwa na Mfuko wa Afya wa Jamii ambao ni mfuko wa hiari wenye lengo la kutoa huduma za afya, ambapo kaya zitakuwa zikilipia huduma hizo na Serikali itatoa mchango wake wa fedha kama jazilio kwa mchango kutoka kwenye kaya; (Tele kwa Tele)

(2) Matumizi ya fedha yatafanywa na kusimamiwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Madhumuni ya Mfuko

5. Madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni:

(a) Kutafuta vyanzo vya fedha kutoka katika jamii kwa ajili ya kutoa huduma bora za afya kwa wanachama;
(b) Kutoa huduma bora za afya zinazopatikana kwa kutumia mipango endelevu; na
(c) Kuboresha huduma za afya katika jamii kwa kugawanya madaraka na kuzipa nguvu jamii katika kufanya maamuzi na kuchangia katika masuala yanayohusu afya zao.

Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii

6. (1) Kutakuwa na Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi baada ya kupokea mapendekezo kutoka Timu ya Wataalam wa Afya wa Halmashauri (CHMT).

(2) Majukumu ya Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii yatakuwa kama ifuatavyo;-

(a) Kufuatilia, kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Jamii kwa kiwango kati ya Halmashauri, Jamii na wadau mbalimbali kwa ushirikiano na mhasibu wa Mfuko; na

(b) Kuandaa taarifa za Mfuko wa Afya ya Jamii za robo mwaka na mwaka kwa kushirikiana na mhasibu wa Mfuko, pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Halmashauri.

Muundo wa Bodi

7. (1) Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao;-

(a) Wawakilishi wanne wa watumiaji huduma za afya kati yao wawili ni lazima wawe ni wanawake.
(b) Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya binafsi bila faida na
(c) Mwakilishi mmoja kutoka watoa huduma za Afya kwa faida waliochaguliwa na Halmashauri kutoka vituo vya kutolea huduma za afya binafsi kwa faida waliochaguliwa miongoni mwao.
(d) Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji.
(e) Afisa Mipango wa Halmashauri
(f) Mganga Mkuu wa Halmashauri ambaye atakuwa Katibu wa Bodi.
(g) Mwakilishi mmoja kutoka Hospitali na Mwakilishi mmoja kutoka Timu ya Uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa.

(2) Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe waliotajwa katika aya (a)-(c) hapo juu.

(3) Wajumbe waliotajwa katika aya (a)-(d) mbali na wajumbe waliotajwa katika aya (e)- (g) za kifungu kidogo cha (1) watakuwa na haki ya kupiga kura katika maamuzi ya Bodi.

Kazi za Bodi

8. Ili kufanikisha malengo yake makuu, Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) itasimamia masuala na shughuli zote zinazohusu Mfuko wa Afya ya Jamii;

(b) itafanya kazi kwa kushauriana na Timu ya Uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa huduma ya afya inayotolewa ni bora na ya kitaalamu;
(c) kukusanya na kusimamia mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii.
(d) kupendekeza kwa Halmashauri watu wanaostahili kusamehewa kutoa mchango kwenye Mfuko
(e) kuweka malengo ya Mfuko.
(f) kupitia ripoti na taarifa kutoka Kamati ya Afya ya Kata au chanzo kingine chochote.
(g) kuratibu makusanyo, matumizi na kudhibiti mapato na;
(h) kupanga mipango ya afya ya mwaka kwa ajili ya kuthibitishwa na Halmashauri.
(i) kupanua na kuongeza utoaji wa huduma za afya kwa wanachama kulingana na mapato ya mfuko;
(j) Bodi katika kutekeleza majukumu yake, itapokea na kutekeleza maagizo ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu

Sifa za wajumbe wa bodi

9. Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo;-
(a) Awe Raia wa Tanzania isipokuwa kwa wawakilishi kutoka katika Taasisi zisizo za Kiserikali.
(b) awe na umri si chini ya miaka ishirini na tano na si zaidi ya miaka sabini;
(c) awe amehitimu elimu ya Sekondari na kuendelea;
(d) awe na uzoefu na amewahi kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma jamii;
(e) awe na sifa za uongozi; na
(f) Asiwe na wadhifa wowote wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa.
(g) Awe mwanachama hai wa Mfuko wa Afya ya Jamii au Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Muda wa kukaa madarakani

10. (1) Mjumbe wa Bodi atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe aliyochaguliwa na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu tu.

*Tangazo la Serikali Na.27 (linaendelea)*

(2) Endapo nafasi yeyote ya mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu, kukiuka maadili ya kazi au ulemavu utakaomfanya ashindwe kushiriki kikamilifu kama mjumbe au kwa sababu nyingine yeyote ile, mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2), haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

Mikutano ya Bodi

11. (1) Mikutano ya kawaida ya Bodi itaitishwa na Mwenyekiti kila robo mwaka.

(2) Ikiwa kuna umuhimu, mwenyekiti anaweza akaitisha kikao cha dharula kulingana na mahitaji maalumu.

Uwajibikaji wa Bodi.

12. Bodi itawajibika kwa Halmashauri kupitia Kamati husika.

Vyanzo vya Mapato

13. Vyanzo vya mapato ya Mfuko vitatokana na:-

(a) Fedha zote zitakazopokelewa kutokana na michango ya wanachama;
(b) Ruzuku kutoka kwenye Halmashauri, Serikali Kuu, na wahisani mbalimbali toka ndani na nje ya Halmashauri;
(c) Michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri
(d) Malipo ya fedha ya wasiokuwa wanachama wa Mfuko kwa kupata huduma ya afya.
(e) Ushuru utakaotozwa na Halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali na kutengwa kwa ajili ya Mfuko; na
(f) Fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata toka mahali pengine popote.

*Tangazo la Serikali Na.27 (linaendelea)*

(g) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

(h) Fedha zozote halali ambazo mfuko unaweza kupata kutoka mahali pengine popote

Akaunti ya mfuko wa Bodi na watiaji saini

14. (1) Kutakuwepo na akaunti maalumu itakayotumika na Halmashauri ambayo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya Mfuko zitahifadhiwa na kutolewa

(2) Malipo yataidhinishwa na Mkurugenzi kwa kufuata taratibu za kanuni za fedha za Halmashauri.

(3) Watia saini wa akaunti ya Mfuko watachaguliwa na Bodi na watakuwa ni mmoja kutoka kundi "A" na "B" na kwa namna yoyote hakuna pesa zitakazotolewa kwenye akaunti ya mfuko bila saini ya mmojawapo kutoka kundi "A" na "B"

(4 Watia saini kwenye hundi za Mfuko watakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekiti wa Bodi na mjumbe mmoja wa Bodi ambao watakuwa Kundi "A"

(b) Katibu wa Bodi (Mganga Mkuu) na Mweka Hazina wa Halmashauri watakuwa Kundi "B"

(5 Kila baada ya miezi mitatu, Bodi itakuwa inatoa taarifa ya akaunti ya Mfuko kwa Halmashauri;

(6 Akaunti ya Mfuko itakaguliwa na wakaguzi waliochaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za fedha za Serikali za Mitaa.

Taarifa ya fedha ya mwaka

15. Mwezi mmoja baada ya mwaka wa fedha wa Halmashauri, Bodi itatakiwa kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha ya mwaka na kuwasilisha kwa Halmashauri.

Mipango na Matumizi

16. (1) Miezi miwili kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha wa Halmashauri, Bodi itaandaa mipango na bajeti ya mwaka kwa kuonyesha kiwango kinachotarajiwa kupatikana na mgawanyo wa fedha kwa ajili ya utoaji huduma za afya na maendeleo katika maeneo ya Halmashauri.

(2) Bodi inaweza kuandaa bajeti ya nyongeza kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo na kama mazingira yataruhusu

(3) Mipango ya bajeti ya Mfuko itaandaliwa kulingana na utaratibu kama ilivyoainishwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) hapo juu, ambayo ni lazima iwasilishwe kwa Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

(4) Matumizi yatazingatia mipango shirikishi ya maeneo husika ambayo itakuwa sehemu ya Mpango kabambe wa afya wa Halmashauri. Pia mipango hii itazingatia maelezo yaliyomo ndani ya Mkataba wa Tele kwa Tele.

Usimamizi wa Mfuko

17. Usimamizi na uendeshaji wa Mfuko utakuwa chini ya :-

(a) Halmashauri kupitia Bodi ya huduma za Afya ya Halmashauri katika ngazi ya Halmashauri.

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata kupitia Kamati ya afya ya Kata, katika ngazi ya Kata; na

(c) Serikali ya Kijiji kupitia Kamati ya Huduma za Jamii katika ngazi ya Kijiji.

Kamati ya Afya ya kata

18. Kutakuwa na Kamati ya Afya ya Kata.

Wajumbe wa Kamati ya Afya ya Kata

19. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Diwani anayewakilisha Kata husika.

(b) Afisa Mtendaji wa Kata;

(c) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka shule ya

*Tangazo la Serikali Na.27 (linaendelea)*

msingi na mmoja kutoka shule ya Sekondari ambayo ipo kwenye Kata husika;

(d) Wajumbe wawili wanawakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe mwanamke.

(e) Mganga au Mganga Msaidizi wa Kituo cha Afya, ambaye atakuwa Katibu wa Kamati.

(f) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutokana na watu waliopendekezwa na Serikali za Mitaa zilizomo ndani ya eneo la Kata; na

(g) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka kwenye vyama vya kijamii kutoka kwenye Kata.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kata atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe.

(3) Endapo Kamati ya Afya ya Kata itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itatoa onyo au kuivunja na kufanya utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe wengine katika muda usiozidi miezi mitatu.

Kazi na Majukumu ya Kamati ya Afya ya Kata

20. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kuwahamasisha na kuandaa jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii.

(b) Kuandaa orodha na kuratibu idadi ya wajumbe wa Mfuko wa Jamii.

(c) Kusimamia ukusanyaji wa michango ya Mfuko.

(d) Kuratibu viwango vya uchangiaji kwenye huduma za afya;

(e) Kupitia utendaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii na kutoa mapendekeo ya ufumbuzi;

(f) Kuanzisha na kuratibu mipango ya Afya ya Jamii na;

(g) Kuendesha mikutano ya wajumbe wa Mfuko wa Afya ya Jamii

(2) Kamati ya Afya ya Kata, itakaa kila baada ya miezi mitatu, na Katibu atatoa taarifa ya maandishi wiki moja kabla ya siku ya Kikao.

(3) Baada ya kikao Katibu atawasilisha muhtasari wa kikao hicho kwa Katibu wa Mfuko wa Halmashauri.

Matumizi ya fedha za Mfuko

21. Fedha zitakazokusanywa na Mfuko zitatumika kwa madhumuni yafuatayo:-

(a) Masuala yanayohusiana na afya yaliyotajwa katika mpango wa afya na kuidhinishiwa na Wizara; na

(b) Suala au shughuli yoyote muhimu ya afya kama itakavyoonekana inafaa na kama itaidhinishwa na Bodi

Utoaji wa Kadi kwa wanachama

22. (1) Kila mwanachama wa Mfuko na wategemezi wake, atapewa Kadi baada ya kulipa mchango wake wa mwaka kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 24(1) cha Sheria Ndogo hizi

(2) Kwa kuzingatia kanuni za Mfuko wa afya ya jamii kila mwanachama atakayepewa msamaha ni lazima atapewa kadi ya uanachama na Halmashauri itaweka utaratibu wa kulipia kadi hiyo.

Haki za mwanachama na Utoaji wa Huduma za afya

23. Kila mwanachama na wategemezi wake watakuwa na haki zifuatazo:

(a) Kupata huduma ya afya aliyolipia anapougua ndani ya eneo la Halmashauri husika au katika kituo cha Afya kwenye Halmashauri nyingine ambayo itaingia makubaliano maalum na Halmashauri husika.

(b) Kupata huduma ya afya kwa baba, mama na watoto wao wenye umri chini ya miaka kumi na nane;

(c) Kutoa mapendekezo kuhusu huduma za afya kupitia kituo chake cha tiba ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi; na

(d) Kushirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa huduma za afya, katika eneo la Halmashauri

Kiwango cha mchango au ada ya mwanachama

24. (1) (a) Mtu yeyote atakayetaka kuwa mwanachama wa mfuko wa afya ya jamii atapaswa kutoa kiasi cha shilingi elfu kumi (10,000) kila mwaka.

(b) Mchango huo utalipwa na kila mtu anayetaka kuwa mwanachama wa mfuko mwanzoni mwa mwaka au kila mwaka wa fedha unapoanza au kama Bodi itakavyoelekeza.

(c) Mtu yeyote ana hiari ya kulipa mchango wake wa uanachama kwa zaidi ya mwaka mmoja;

(2) Bila kuathiri kifungu cha 24 (c) hapo juu mtu yeyote anayelipa mchango wa uanachama kwa zaidi ya mwaka mmoja, pale inapotokea mabadiliko ya kiwango cha mchango atawajibika kulipa tofauti ya kiwango kilichozidi kile cha awali.

(3) Halmashauri itaandaa utaratibu wa kupanga kaya maalum zilizoko katika Taasisi/Shule mbalimbali zilizo ndani ya Halmashauri ili kuziwezesha kupata huduma ya mfuko wa Afya ya jamii.

Muda wa uanach-ama

25. (a) Mtu yeyote atabaki kuwa mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii wa kila atakapolipa ada yake ya mwaka.

(b) Kila mwaka unapoisha uanachama wa mtu utafikia mwisho hadi pale atakapotimiza masharti ya kifungu cha 25 (a) hapo juu.

Malipo ya papo kwa papo

26. (1) Mtu yeyote ambaye hatakuwa mwanachama wa mfuko huu, atalipa mchango au malipo ya papo kwa papo kila

atakapoenda kupata matibabu katika kituo cha kutolea huduma za Afya.

(2) Malipo ya papo kwa papo yatalipwa kama ifuatavyo;
- (a) Shilingi elfu moja (1,000/=) katika huduma za afya zinazotolewa na Zahanati katika eneo lolote la Halmashauri.
- (b) Shilingi elfu moja mia tano (1,500) kwa huduma za Afya zinazotolewa na kituo cha Afya kilichopo ndani ya Halmashauri.
- (c) Huduma za Hospitali za aina zote kulingana na Sera ya uchangiaji.

Misamaha kwa wasiojiweza

27. Misamaha kwa wasioweza kulipa gharama za matibabu itatolewa na kulipwa na Halmashauri baada ya kuzingatia utaratibu ufuatao;-
- (a) uongozi wa Kitongoji utawatambua, kuwaorodhesha na kuwasilisha majina ya wasio na uwezo wa kulipa gharama za matibabu katika Serikali ya Kijiji;
- (b) Serikali ya Kijiji katika vikao vyake itapokea, itajadili na kuwasilisha orodha sahihi kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata;
- (c) Kamati ya Maendeleo ya Kata itapokea,itajadili na kuwasilisha orodha sahihi ya wasioweza kulipa gharama za matibabu kwa Bodi ya Afya ya Halmashauri; na
- (d) Bodi ya Afya itapokea, na kujadili mapendekezo husika na kuyawasilisha pamoja na gharama zake kwa Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi.

Makosa

28. Itakuwa ni makosa kwa mtu yeyote ambaye;
- (a) Atakwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi; au
- (b) Atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi kufanya kazi zake kwa ufanisi; au
- (c) Atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko na

*Tangazo la Serikali Na.27 (linaendelea)*

kusababisha kutofikia malengo ya Bodi; au

(d) Atatumia vibaya madaraka aliyonayo kumzuia afisa wa Bodi kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii;

(e) Atashindwa kwa uzembe kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi.

*Adhabu* 29 Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele imebandikwa katika Sheria hizi Ndogo kutokana na Azimio la kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kilichoketi tarehe 17 mwezi 07 mwaka 2015 na lakiri imebandikwa mbele ya:-

GODWIN L. BENNE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

DUES J. BUNDALA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*